# OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA ( OR –TAMISEMI )

## HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBWANGA

SHULE YA SEKONDARI CHANJI
S.L.P 335,
**SUMBAWANGA**

**SIMU 0757784599**

**TAREHE.............................**

**MZAZI / MLEZI WA MWANAFUZI..........................................................................**

**YAH: KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHANJI WILAYA YA SUMBAWANGA MANISPAA, MKOA WA RUKWA MWAKA...........................**

Ninayofuraha kukuarifu kuwa mwanao ……………………………………………………

Aliyekuwa akisoma Shule ya Msingi ……………………………………………Mwenye namba ya mtihani PS………………………………………… amechaguliwa na Bodi ya Uchaguzi ya Mkoa wa Rukwa kujiunga na Shule ya Sekondari Chanji iliyopo kata ya Msua, Mtaa wa Kisiwani katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga

Aidha Shule itafunguliwa tarehe………………………………… Mwanao atatakiwa kufika/kuripoti Shuleni bila kukosa tarehe hiyo,vinginevyo nafasi yake itachukuliwa na mwanafuni wa akiba baada ya siku saba.

Nakutakia maandalizi mema

**...............................................**
**MKUU WA SHULE**

## SHULE YA SEKONDARI CHANJI
## MAMBO YA MUHIMU YA KUZINGATIA

**A: SARE YA SHULE**

**I)WAVULANA**

**SURUALI**:- Anatakiwa ashone suruali mbili (2), moja yenye RANGI YA KIJIVU na nyingine yenye RANGI YA UGORO ,ikiwa na mifuko ya kawaida na rinda mbili kila upande, **Mifuko ya kubandika hairuhusiwi na pia suruali za kubana (Modo) haziruhusiwi kabisa hapa shuleni**

**SHATI:-**Awe na mashati mawili (2) yenye mikono mifupi (short sleeves)

**VIATU**;- Awe ana viatu vyeusi vya ngozi visivyo na sori ndefu vyenye Kamba na visivyochongoka kwa mbele vinavyovaliwa na soksi za rangi nyeusi fupi.

SWETA:- Awe na sweta la rangi ya Ugoro yenye shingo "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi.

**SARE ZA MICHEZO**:- Awe na Bukta,T-shirt n raba za michezo jozi mbili za Trachsuit nyeusi

**II)WASICHANA**

**SKETI**:Anatakiwa kuwa na sketi Mbili (2) moja **YA RANGI YA KIJIVU** na nyingine yenye **RANGI YA UGORO** na ishonwe sketi ya marinda na ni lazima ziwe ndefu kuvuka magoti

**SHATI:-** Awe na mashati mawili (2) yenye mikono mifupi (Short sleeves) .Kwa waislam,,Hijab ziwe na rangi nyeupe sawa na mashati

**VIATU:** Awe ana viatu vyeusi vya ngozi visivyo na sori ndefu vyenye Kamba na visivyochoongoka kwa mbele vinavyovaliwa na soksi na rangi nyeupe fupi.

**SWETA:** Awe na sweta rangi ya Ugoro shingo ya "V" kwa ajili ya kujikinga na baridi

**SARE ZA MICHEZO**: Awe na sketi,Fulana,(Tshirt) n raba za michezo jozi mbili (2) na Tracksuit nyeusi

**NYWELE:-** Hakuna kusuka nywele ziwe fupi

***NB:- Ni vyema Mzazi/Mlezi ukafika shuleni kupata maelekezo ya sare ili kuepuka kununua sare kinyume na zilizoelekezwa kwani hazitakubaliwa na kuingia gharama ya kununua nyingine***

**B: VIFAA VYA USAFI**

1.Ndoo lita 10
2. Mifagio yenye mpini mirefu 01
3.Jembe moja lenye mpini
4.Fyekeo 1

**C: VIFAA VYA MASOMO**

1. Daftari kubwa (Counter books) Zisizopungua 12
2. Mathematical set 1 (Mkebe)
3. Kamusi ya kiingereza 1 (Dictionary)
4. Kalamu,rula na penseli

**D: VITU VINGINE VYA MSINGI ANAVYOTAKIWA KUWA NAVYO MWANAFUNZI**

1. Anatakiwa awe na T.shirt 1 itakayokuwa na nembo ya MOTTO wa shule ambayo ni sehemu ya sare inayovaliwa siku ya usafi shuleni (Ili kuepusha utofauti wa sare inashauriwa kupata maelekezo Zaidi Shuleni)
2. Aje na Picha- Pasport size Nne 4 zilizopigwa mwanafunzi akiwa amevaa sare za shule nyuma kuwe na rangi ya bluu
3. Anatakiwa awe na nembo ya shule ambayo itabandikwa kwenye mfuko wa shati ili kumtofautisha na mwanafunzi wa Shule nyingine
4. Aje na mti mmoja kwa ajili ya kupanda ili kutunza mazingira ya shule

**OFISI YA RAIS –TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**(OR – TAMISEMI )**

# A. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyoboreshwa kwa sharia Na.10 ya mwaka 1995.Aidha ,inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ,yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya waziri mkuu –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu .Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

a) **Heshima** kwa viongozi ,wazazi,wafanyakazi wote wa shule ,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la **lazima.**
b) mahudhurio **mazuri** katika kila shughuli ,ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni la **lazima.**
c) **Kuwahi** katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa /kupangiwa.
d) **Kufahamu mipaka ya shule** na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka ya shule **wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.**
e) Kutunza usafi wa mwili ,mavazi na mazingira ya nje.
f) **Kuvaa sare ya shule wakati wote** unapotakiwa na kwa kuzingatia siku na rangi ya sare kwa siku hiyo.
g) **Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.**
h) Kutunza mali za shule na umma kwa ujumla na katika ofisi za serikali.

**B: MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE**

a) Wizi
b) Uasherati na na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi,cocane, mirungi , kubeli ,uvutaji wa sigara na kadharika
e) Kupigana na kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya shule na umma kwa ujumla
g) Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa na nembo nyingine zinazolitambulisha Taifa
h) Kuwa mjamzito/Kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma,kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

Kujihusisha na vitendo vya mapenzi shuleni ni kosa la kufukuzwa shule

**E:MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule atakaporudi Shuleni (***FOMU HII ITAJAZWA OFISI YA MKURUGENZI MANISPAA YA SUMBAWANGA NA SI VINGINEVYO***)
b) Fomu ya maelekezo binaafsi kuhusu historia ya wanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika Migomo,fujo na makossa ya jinai
c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubalina na sharia , kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule
d) Fomu ya udhibitisho wa uraia wa mwanafunzi na cheti cha kuzaliwa aje na kopi kama mbadala wa hiyo fomu ya udhibitisho wa uraia

N***B:Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.***

## KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CHANJI

# “OUR MOTTO – EDUCATION FIRST”

…………………………………………………….

**MKUU WA SHULE**